

# MASOKO SECONDARY SCHOOL

S.L.P 303,

TUKUYU.

**Mob: 0752637958**

**Tarehe.....**

Kumb. Na.....

Jina la mwanafunzi.....

S.L.P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASOKO WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2020/2021**

## **1.0 utangulizi**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kijiunga na kidato cha **Kwanza** katika shule hii mwaka 2021 Shule ya sekondari **Masoko** ipo umbali wa **km 09 Magharibi** mwa Mji Mkuu wa Tukuyu katika Wilaya ya **Rungwe** Mkoa wa **Mbeya**.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021na mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2021

## **2.0 Mambo mhimu ya kuzingatia**

### **2.1 Sare za shule**

(A)Sare ya shule ni **suruali 2(i) Rangi ya damu ya mzee (ii) Nyeusi kwa wavulana .Na sketi 2 (i) rangi ya damu ya mzee na nyeusi rinda 16 na ndefu kupita magoti, shati mbili nyeupe za tetroni mikono mifupi kwa wote(wavulana na wasichana)**. Sweta lifuate rangi ya sare, viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kamba,soksi nyeupe jozi mbili kwa wasichana na soksi jozi mbili kwa wavulana

(B) Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule

(c) Sare ya michezo ni trak sut nyeusi kwa wasichana, bukta na fulana njano kwa wavulana

### **2.2 Vifaa vya taaluma**

- |   |                   |       |
|---|-------------------|-------|
| ❖ hisabati(mathematical set)            | Vifaa             | vya   |
| ❖ kumi na mbili(2&3quire)               | Daftari           | kubwa |
| ❖ i za kuhifadhia taarifa za mwanafunzi | Peni,penseli,fail |       |

## **2.3 viiaa vya usafi**

<b>i.</b>		Ndoo
<b>ii.</b>	slesha(kwanja)	Jembe
<b>iii.</b>		Fagio
<b>iv.</b>		Mopper

## **2.4 Chakula**

Chakula cha wanafunzi kwa shule za kutwa ni mhimu kwani humjengea mwanafunzi uwezo mzuri wa kufikiri,kupunguza utoro, Hivyo kutohana na muongozo kila mzazi anajukumu la kumfanya mtoto wake anapata chakula baada ya makubaliano na kikao cha wazazi.

## **3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule**

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria Elimu Na.**25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na **10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Raisi- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- a. Heshima kwa viongozi ,wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shulenii ni lazima
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni
- d. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa kama mwanafunzi katika shule hii
- f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i. Kutunza mali za umma

### **3.1 makosa yaifuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule**

- a) Wizi**
- b) Uasherati na ushoga**
- c) Ubakaji**
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi kubeli na kadhalika**
- e) Kupigana au kupiga**
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma**
- g) Kudharau bendera ya Taifa**
- h) Kuwa mjamzito au kupata mimba**
- i) Kuoa au kuolewa**
- j) Kutoa mimba**
- k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu**
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi**
- m) Kuwa na simu ya mkononi**

### **3.2 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulenii na mwanafunzi**

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serkali**
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na mkosa ya jinai**
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.Fomu hizo zimeambatanishwa kwenye fomu hii**

### **3.3 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA SHULENI MASOKO**

.....

**MKUU WA SHULE**